

Jifunze kitu kupitia kisa hiki cha mume na mke

By SW - Melkisedeck Shine · January 12, 2015

Baini Siri za Familia, Mapenzi na Mahusiano · #Karibu AckySHINE · #Mahusiano: Makala kwa Mke na Mume · #SMS, Vichekesho, Mahusiano, Biashara na Ujasiriamali, Afya, Chemsha Bongo, Dini pamoja na Vitabu kwenye PDF

Mwanaume mmoja alimuoa mwanamke mrembo. Alikuwa akimpenda sana. Siku moja mwanamke alipatwa na maradhi ya ngozi. Kidogokidogo alianza kupoteza urembo wake. . . .

Mume alipata safari na wakati akirudi alipata ajali iliyomfanya apoteze uwezo wake wa kuona. Hata hivyo, maisha yao ya ndoa yaliendelea kama kawaida. Lakini kadiri siku zilivyosonga mbele ndivyo mke alivyoendelea kupoteza urembo wake. Kwa kuwa mume alikuwa kipofu hakulijua hilo na hivyo hakuna kilichobadilika kwenye upendo wao. Aliendelea kumpenda, na mke alimpenda sana mumewe. . . .

Siku moja mke alifariki dunia. Ilikuwa huzuni kubwa sana kwa mume. Baada ya kumaliza taratibu zote za maziko, mazishi na kutandua msiba, alipanga kuhama kwenye mji huo na kwenda kuishi kwenye mji mwingine. . . .

FUNZO:

Wakati fulani ni vizuri ukajifanya kipofu na kuyapuuza mapungufu ya mwenzako ili kumfanya awe mwenye furaha.

1. Ukiwa peke yako unaweza kuongea, lakini ukiwa pamoja na mwenzako mnaweza KUZUNGUMZA.
2. Ukiwa peke yako unaweza KUFURAHIA, lakini ukiwa na mwenzako unaweza KUFURAHIA.
3. Ukiwa peke yako unaweza KUTABASAMU, lakini ukiwa na mwenzako mnaweza KUCHEKA.

Huo ndio UZURI wa mahusiano yetu kama binadamu. Tunategemeana.

Kiwembe kina ukali lakini hakiwezi kukata mti; shoka lina nguvu na imara lakini haliwezi kukata nywele.

*Kila mtu ni muhimu kulingana na kusudio na lengo la uwepo wake. Usimdharau mtu yeyote kwa hali yoyote, kwa sababu huwezi kuwa yeye.

Mwenyezi Mungu atujaalie nguvu na moyo wa kusamehe, kustahmilia na kuishi kwa umoja. . Tafakari Mm na ww tunaweza kufanya haya!!!

Yafhamu Mambo Mbalimbali kuhusiana na Wanawake kwa Ku-Download Kitabu cha SIRI ZA MWANAMKE

Kitabu hiki kina topiki Zifuatazo; 1. Mambo anayohitaji mwanamke kutoka kwa Mwanaume 2. Mambo yanayowavutia wanawake kutoka kwa wanaume 3. Mambo wanayoyapenda wanawake wakati wa kufanya mapenzi 4. Dalili za mwanamke kicheche 5. Maswali ya kujiuliza kama mwanamke anakupenda kwa dhati au anakudanganya 6. Tabia za mwanamke anayekupenda lakini hawezi kusema 7. Ishara za mwanamke aliyevutiwa na wewe 8. Dalili za mwanamke

anayeelekea kukukubali 9. Mambo ambayo mwanamke hawezi kukwambia 10. Njia za kudumisha na kuamsha mapenzi na mwanamke

[products columns="2" ids="30827"]

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=3296>